# FURAHA YA KWELI NA AMANI YA NDANI

**Ukadiriaji:**

**Maelezo:** Jinsi Uislamu unavyofafanua furaha ya kweli na amani moyoni.

**Aina:** Makala Manufaa ya Uislamu Furaha ya kweli na Amani ya Ndani kwa Ndani

**Na:** islam-guide.com
**Iliyochapishwa mnamo:** 03 Dec 2021
**Ilirekebishwa mara ya mwisho mnamo:** 18 Nov 2021



Furaha ya kweli na amani inapatikana kwa kutii amri za Muumba na Mtegemezi wa ulimwengu huu. Mungu amesema katika Kurani:

***"Kwa kweli, katika kumkumbuka Mungu moyo hupata raha na utulivu." (Kurani 13:28)***

Kwa upande mwingine, yule ambaye hatakifuata kitabu kitukufu atakuwa na maisha ya shida katika ulimwengu huu. Mungu amesema:

***" Atakayeiacha Qur'ani,[1] atakuwa na maisha magumu, na tutamfufua kipofu katika siku ya Kiyama." (Kurani 20: 124)***

Hii inaweza kuwa kielelezo ni kwanini watu wengine hujiua wakati wanafurahia raha ya mali inayoweza kununuliwa na pesa. Kwa mfano, angalia Cat Stevens (sasa Yusuf Islam), zamani alikuwa mwimbaji maarufu wa 'pop' ambaye alikuwa akipata zaidi ya dola 150,000 kwa usiku. Baada ya kusilimu, alipata furaha ya kweli na amani, ambayo hakupata katika mafanikio ya mali.[2]

---

Rejeleo la maelezo:

[1] Yaani haamini Kurani wala haitii amri zake.

[2] Anwani ya barua ya sasa ya Cat Stevens (Yusuf Islam), ikiwa ungependa kumuuliza juu ya hisia zake baada ya kusilimu, ni: 2 Digswell Street, London N7 8JX, Uingereza.

Anwani ya wavuti ya makala hii:

https://webcache001.islamreligion.com/sw/articles/244/furaha-ya-kweli-na-amani-ya-ndani

Hakimiliki © 2006-2020 Haki zote zimehifadhiwa. © 2006 - 2026 IslamReligion.com. Haki zote zimehifadhiwa.